

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

SHULE YA SEKONDARI KIBWIGWA

S.LP 206

BUHIGWE,KASUILU

13/12/2021

JINA LA MWANAFUNZI;

YAH: MAAGIZO YA KUHUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBWIGWA WILAYA YA BUHIGWE
MKOA WA KIGOMA MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafuraha kukutarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Kibwingwa ipo umbali wa kilometer nane magharibi mwa mji mkuu wa haimashauri ya wilaya Buhigwe. Masomo ya mhura wa kwanza yanatarajia kuanza tarehe.../1/2021 Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe/1/2021 hadi tarehe.../1/2021 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule;

a) Wavulana suruali blue bahati pea mbili (2) na shati nyeupe mnili (2) mikono mifupi, viatu vyeusi vya ngozi na vya kufunga na kamba, soksi nyeupe, Sweta rangi ya kijani na tisheti rangi ya damu ya mzee ambayo utapewa maelekezo shuleni namna ya kuipata. Pia mshono wa suruali ni rinda mbili na isiyobana

b) Wasichana siketi rangi blue bahati pea mbili shati nyeupe mbili [(2) mikono mifupi, soksi nyeupe, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na vya kufunga na kamba, Sweta rangi ya kijani na tisheti damu ya mzee ambayo utapewa maelekezo shuleni namna ya kuipata. Pia mshono wa sketi ni rinda box, sketi ndefu na isiyobana.

2.2 Vifaa vya darasani;

Vifaa vya darasani kama ifuatavyo;

1. Madaftari makubwa kumi (10) counter book

2. Rula ,penseli, kalamu za kutosha na mkebe wa hesabu

3. Kamusi (DICTIONERY) ya kingereza kwa Kingereza.

2.3 Mahitaji mengine ya kuja nayo;

Aidha mahitaji mengine ya kuja nayo ni kiti na meza pamoja na shilingi 6000 ya t-shirt na shilingi 10,000 ya sweta.

3.0 Sheria na kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na .25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa Kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na I2ara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

a) Heshima kwa viongozi ,Wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c) Kushiriki kwa umakini kufanya maandario yá jioni (Night preparation).

d) Kuwahi katikà kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

e) Kufahamu mipaka ya shule nakuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwapo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

f) Kutunza usafi wa mwil, mavazi na mazingira ya shule.

) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

i) Kutunza mali za umma

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha tufukuzwa au kusimamishwa shule

a) Wizi

b) Uasherati na ushoga

c) Ubakaji

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile; Uvutaji bangi, cocaine, mirungu, kubeli na kadhalika

e) Kupigana au kupiga

f)Kuharibu kwa makusudi mali za umma.

g)Kudharau Bendera ya taifa

h)kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha ujauzito.

l) Kuoia au kuolewa

j) kutoa mimba Kugoma.

k) kuhoma,Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu na mali zao.

l)Kukataa adhabu kwa makusudi

m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na uwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Madical examination form arnbayo itajazwa na mganga mkuu hosipitali ya serikali. Form hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni

b)Form ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa nashule.

5.0 Tafadhali soma makini maelezo/ Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SAANA KATIKA SHULE HII

Mkuu wa shule